BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 19 Mei, 2022
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

92. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwa kuwa Baraza la Mji la Chake chake limefikia vigezo vya kuwa Manispaa, na kwa kuwa Serikali ilitoa ahadi ya kulipandisha hadhi Baraza hilo na kuwa Manispaa, na kwa kuwa muda mrefu sasa umepita bila ya ahadi hiyo kutekelezwa.

Je, ni hatua gani imefikiwa katika utekelezaji wa ahadi hiyo.

### Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

176. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) ni miongoni mwa taasisi muhimu katika kuhakikisha ubora wa bidhaa na huduma zinazoingia na zinazozalishwa Zanzibar hasa kuelekea utegemezi wa Uchumi wa Buluu ambapo kutahitajika bidhaa zenye ubora wa Kimataifa ili bidhaa za Zanzibar, zikiwemo za baharini, ziweze kupenya kwenye soko la dunia. Hata hivyo, ZBS

inakumbwa na changamoto nyingi kiasi kwamba imekwama kupata uanachama wa ISO na kupata ithibati.

(a) Je, ni lini Serikali itaajiri wafanyakazi wa kutosha wakiwemo wenye taaluma za viwango ili kufikia viwango vinavyokubalika na ISO.

(b) Je, ni lini Serikali itaiwezesha ZBS kisheria na kirasilimali watu kuweza kukagua ubora wa mizigo inayoingia Zanzibar kupitia bandari rasmi na bandari bubu na viwanja vyote vya ndege.

(c) Je, ni lini Serikali itaipatia ZBS eneo na ofisi ya kutosha katika bandari zote na kwenye viwanja vya ndege ili iweze kufanya kazi zake za ukaguzi na udhibiti wa viwango kwa ufanisi zaidi.

**<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>**

159. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Nchi nyingi hivi sasa duniani zimekuwa na utaratibu wa kuwapeleka ughaibuni vijana wenye vipaji vya mpira wa miguu kwa ajili ya kufanyiwa majaribio kupitia mawakala wa ndani na wa nje.

(a) Je, mpaka sasa Zanzibar tuna mawakala wangapi ndani na nje ya nchi wanaojishughulisha na suala hilo.

(b) Ni lini Wizara yako italisimamia jambo hilo angalau kuwadhamini kwa fedha ili waweze kurejesha baada ya kufuzu majaribio yao kwa utaratibu maalum vijana hao.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

170. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Wananchi wa jimbo la Pandani wanatoa shukrani na pongezi kwa Serikali kwa ziara zilizofanywa na Mheshimiwa Rais na Makamo wake kwa nyakati tofauti katika bonde la kilimo cha juu la Tovuni na kuahidi ujenzi wa ukuta wa kuzuia chumvi kuingia mashambani ambao tayari umejengwa kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, wakati wananchi wakisubiri utekelezaji wa ahadi hiyo, kulitokea uharibifu mkubwa wa chumvi kuvamia

mashamba ya wananchi wanyonge na kuharibu mbegu zao.

(a) Je, Serikali imetathmini na kujua gharama za uharibifu huo wa karibuni ndani ya 2021/2022.

(b) Je, Serikali haioni haja kuwapa ahueni wakulima hao kwa kuwapatia ruzuku ya angalau mbegu, dawa na mbolea.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kujenga miundombinu ya kijamii katika maeneo ya bonde hilo ili kuhamasisha maendeleo ya kilimo katika eneo hilo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

107. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika skuli ya Jeshi la Wananchi ya Ali Khamis Camp 14kj kuna tatizo kubwa la maabara za Physics, Chemistry na Biology jambo ambalo hupelekea wanafunzi wake kufanya elimu ya matendo katika skuli ya jirani ya Fidel Castro.

(a) Je, jambo hili ni kweli.

(b) Kama ni kweli, ni lini Serikali itatoa msaada wa moja kwa moja au kupitia wafadhili katika ujenzi wa maabara hizo ukitilia maanani zaidi ya asilimia 80 ya wanafunzi wake ni watoto wa wakulima na wakwezi.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

119. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Serikali inastahili pongezi kwa kutambua uwepo wa vijiji vya Jitenge na Tundaua ndani ya jimbo la Pandani na kuvipelekea baadhi ya huduma za kibinaadamu. Hata hivyo, kwa siku za karibuni, vijiji vya Jitenge na Tundaua vimesahauliwa sana na kukosa huduma muhimu za kimaendeleo zikiwemo huduma za maji.

(a) Je, Serikali inatambua huduma gani rasmi ya maji kwa watu wa vijiji vya Jitenge na Tundaua.

(b) Kwa kuwa mifumo ya maji ya kisima cha UNICEF ndani ya kijiji cha Jitenge imeharibika, Je, ni lini Serikali itawatengenezea mifumo rasmi ya maji watu wa Jitenge na watu wa Tundaua ambao hawana mifumo ya maji

rasmi kabisa.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kudhibiti na kutathmini ubora wa mifumo ya maji vijijini ili kuhakikisha huduma ya maji inakuwa endelevu na salama.

## II. HOJA ZA SERIKALI:

### Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka 2022/2023.

**Zanzibar,**
**19 Mei, 2022.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**